Kama tulivyosoma kwenye Biblia tumeona kwamba watumishi wote wa Mungu walikuwa na majaribu (trials )na majanga ambayo yaliwapata kwa namna tofauti tofauti kipindi chote cha uhai wao. Mungu hutumia hari za maisha yetu kujaribu imani yetu na upendo wetu kwetu. Majaribu yetu yaweza kuwa si kama yale yaliyo mpata Yusufu alipouzwa misri, au Daudi alipo kuwa anatafutwa na sauli, au Danieli alipotupwakwenye shimolilikuwa na samba au rafiki zake watatu ambao walitupwa katika tanuru la moto lakini watumishi wa Mungu wote watakuwa na majaribu ya namna mbalimbali .Je, tunaamini kwa moyo wote kwamba siku zote Mungu anatulinda ili kutusaidia au tutamuacha Mungu tunakuwa kwenye shida na kuchukua njia Fulani ya mkato?Paulo ambaye alivumilia sana mateso alipokuwa akiendelea kuhubiri Injili aliwambia waumini akiwaonya "wakae katika ile Imani nay a kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi (Matendo 14:22).

Imani yetu inaweza kuwekwa katika jaribio katika kufanya msimamo wa dhamili safi dhidi ya sheria zinazo onyesha kuturazimisha kuziacha njia za Mungu. Inaweza ikawa kwamba tuna matatizo ambayo ni vikwazo kwetu, Majaribu yanaweza kuja kazini kwasababu ya imani yetu au kwenye nyumba zetu kutoka kwa wale wasio amini kama sisi tunavyo amini. Inaweza kuwa tumetengwa kutoka kwa waumini wengine na kujisikia wapweke humu Duniani kuna namna nyingi ambazo kwa hizo imani yetu na upendo wetu hujaribiwa .Hatshuvyo katika kila hali ni lazima siku zote lukumbuka kwamba Mungu mwenyewe hujua matatizo yetu na atasikia maombi yetu tunapojibidisha kufuata mfano na matendo kama ya kristo.

Majaribu ni nafasi ya kuonesha Imani yetu katika Mungu yakobo aliandika “Ndugu zangu hesabuni ya kuwa ni furaha tupu mkiangukia katika majaribu mbalimbali mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta sabuni sabuni na iwe na kazi kamilifu mpate kuwa wakamilifu na watilifu bila kupunguliwa na neno” (yakobo 1:2-4) petro aliona jaribu la imani kama vile usafishaji wa dhahabu na alionesha kuomba tabia zetu husafishwa au huimarisha kuomba tabia zetu husafishwa au huimarishawa kwa kile tunachovumilia na kushinda :”ili kwamba kujaribiwa kwa Imani yenu ambayo inathamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo yapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto kuonekana kuwa kwenye sifa ni utukufu na heshima katika kufunuliwa kwake yesu kristo “ (1 Petro 1:7 )

Hapa kuna baadhi ya manukuu ya kutia moyo ambayo yanaweza kutusaidia wakati wowote tunapojifika kuelewa au kuwa na matatizo:

“Wapenzi ,msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu unaowapata kama moto ili kuwajaribu kama kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho.Lakaini kama mnavyoyashiriki mateso ya kristo furani ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe”(1 petro 4:12-13).Petro aliandika maneno haya kwa sababu wanafunzi walikuwa wakipata mateso mengi vikiwemo vifa kwa watawala na kirumi wapagani kwa sababu ya imani yao katika kristo Anaongozea endapo mtu yeyote anateseka akiwa ni mkristo “asione haya bali amtukuza Mungu katika jina hilo” (Mstari wa 16)

Maongezi yako yasiwe ya kutamani (au kuombaomba vitu ) ridhika na alivyonavyo kwani amesema “sitakupungukia kabisa wala sitakuacha kabisa Bwana ndiye anisaidiaye sitamwogopo mwanadamu atanitenda nini.”(waebrania 13:5 -6). Kinachotakiwa ni kujua Mungu latakuacha hata kama kuna majaribu ya namna gani mradi tumtegemee yeye. Kuna nyakati ambazo tutajihisi kutokuweza kushughulika na yanayotupata lakini tuna uthibitisha huu kutoka kwa Paulo : Jaribu halikuwapata isipokuwa lililokawaida ya wanadamu ila Mungu ni mwanafunzi ambaye hatawaacha nyaribiwe kupita mwezavyo lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea ili mweze kustahilimili “ (1 wakorintho 10:13)

Hapa kuna baadhi ya maneno kutoka zaburi ambayo huweza kutusaidia katika nyakati kama hizo.

“Siku ya hofu yangu nitakutumaini wewe. Kwa msaada wa Mungu nitalisifu neno lake Nimemtumaini Mungu sitaogopa ;Mwenye mwili atanitenda nini” (Zaburi 56:3-4).

“Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara ,Maana wewe Bwana peke yako ndiwe unijaliaye kukaa salama “ (Zaburi 4:8).

“Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari “(Zaburi 46:1-2)

“Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa naam ngome kwa nyakati za shida Nao wakujuao jina lako watumaini wewe maana wewe Bwana hukuwaacha wakutafutao “ (Zaburi 9:9-10).

Zaburi hizi ni maombi yanayotuonesha sisi jinsi watu waaminifu hapo zamani walivyomgeukia Mungu walipokabiliwa na matatizo makubwa nyakati kadhaa.Tunapokumbwa na majaribu tunahitaji kuwa makini kutafuta msaada wa Mungu katika maombi. Ni lazima tufuate ushauri wa Petro, alipo sema, “mkitumika yeye fedha zenu zote, kwamaana yeye hujishughurisha sana kwa mambo yenu.” (1 Petro 5:7).

Hata tupate shida vipi kwa ajili ya imani yetu, iwe ni mateso au dhiki au upweke au matatizo ya aina yoyote ile, hata kuja kujua kuwa wengine pia wamepata shida hizi.Tunaweza jifunza kujua mahitaji yao na hivyo kujikuta kuwa tunaweza kuwasaidia na kuwatia moyo pia. Katika moja ya mifano aliyo toa yesu alionyesha kwamba katika ufalme walikuwa ni wale waliowatembelea na kuwatunza ndugu zao waliokuwa wakiteseka: "ndipo wenye haki watakapo mjibu, wakisema, Bwana , na hivi tulipo kuwa na njaa ulitushibisha, au una kiu ukatunywesha?NI lini tena tulipo kuona umgonjwa, au kifungoni, tukakujia?Na mfalme atajibu, akiwaambia; Amn nawambia, Kadri nilvyo mtendea mmoja wapo wa hao ndugu zangu walio wadogo mlinitendea mimi." ( Mathayo 25:37-40 ).

Maadam wanafunzi wote hupata shida au magumu kwa namna moja au mjipime, hebu tutiwe moyo kwa maneno ya Paulo : "Kwamaana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakao simuriwa kwetu ." tukijua ya kwamba "katika mambo yote ya Mungu hufanya kazi moja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa na kwa kusudi lake." Kwamaana hakuna kitu chochote ambacho kitaweza "kututenga na upendo wa Mungu ulio katika kristo Yesu Bwana wetu." (Waumini 8:18,28, 38-39 ). Tuna waaminifu, hivyo Mungu atakuwa pamoja nasi na kamwe hatatuacha bila kujali ni magumu kiasi gani yatatupata.

HITIMISHO.

Tunatumaini kwamba hayo hayo juu yanaweza kutoa mwongozo na kutia moyo tunapo fuata maelekezo ambayo Mungu alituachia ili tumfuate. Kwa muhtasari, endapo jaribu linainuka au tunatatizwa tunapo fanya maamuzi; moja ya maswari rahisi tunawezakujiuliza ni : "Endapo yesu kristo alikuwa pamoja nami sasa, je ungefanya kitu hiki? Au ningeenda kule waliko niomba au kutaka niende? Je ningetegemea yesu kuwepo kwenye sehemu kama hii?Je ninge kuwa na furaha kukaa na kutazama filamu hii au kusoma kitabu hiki endapo yesu yupo nami? Ufuasi wa yesu unapaswa kuwa wa mazoea kama hayo.

Paulo analiweka swala hili kwa namna hii ; "basi ikiwa mmefufuliwa pamoja na kristo yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko keti mkono wa kiume wa Mungu yafikirini yaliyo juu sio yaliyo katika nchi." (Wakorosai 3:1-2 ) Mfuasi wa yesu tayari amesha kufa kwa mwenendo wa maisha ya zamani ya mwili kwa sababu ya ubatizo nasasa amefufuriwa katika kristo. Akili yetu Paulo asema inatakiwa kuwa katika hali hiyo ya utakatifu ambapo Yesu yupo upande wa kuume wa Mungu.

Kama tulivyo eleza hapo mwanzo,Paulo amesema : "Itoeni miili yetu.

.Iwe dhabihu iliyo hai,Takatifu ya kumpenza Mungu, Msifuatishe namna ya dunia hii, Bali mgaw kwa kufanywa upya nia zenu "(Warumi 10:1-2)

Tunahitaji akili zetu kuzama kwenye mambo yenye manufaa yanayo mpendeza Mungu.

Kwa hitimisho hebu tufikilie ushauri wa Paulo :

" Upole wenu ujulikane kwa watu wote . Bwana yu karibu msijisimbue kwa neno lolote ; bali katika kila neno na kusari na kuomba, Pamoja na kushukuru , haja zenu na zijulikane na Mungu Na amini ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika kristo Yesu. Hatimaye ndugu zangu mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote ya kumpendeza, yoyote yenye sifa njema, ukiwepo wema wowote, ikiwepo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo." (Wafilipi 4:5-8 ).

Mungu akubariki katika usomaji wako wa neno lake na itakuwa kwamba utafurahia majaribu ya wokovu ambayo Mungu amekujaria ubatizo katika Yesu kristo, na kumfuata kwa utiifu.

**NIFANYE NINI?**

Sasa tumefikia mwisho wa safari yetu ya kuichambua Biblia kwa kutumia maneno haya kama mwongozo. Kozi yetu imetuchukua kutoka kwenye uumbaji mpaka siku ya Bwana Yesu kristo na mitume. Tumeona jinsi dhambi ilivyo ingia ulimwenguni, ukaleta kifo kwa Adamu na uzawa wake wote. Hata hivyo nimeshangaa kuona namna Mungu kwa hekima yake na rehema yake alivyo toa msingi wa msamaha wa dhambi na kutoa tumaini la uzima wa milele kupitia kazi ya Bwana yesu kristo.

Hatujafuata historia ya biblia tu, bali tumeona jinsi Mungu, kupitia manabii wake, amefunua lengo tukufu wa kuusimamisha ufalme wake katika dunia hii chini ya utawala wa Bwana Yesu kristo na watumishi wake waaminifu. Tumevutiwa na wingi wa unabii unao husiana na siku zetu na utimilifu wao. Unabii huu, pamoja na ule uliotimia tayari katika kihistoria kuthibitisha kuwa Biblia nimepulizwa na hutupatia mwamko na uhakika kwamba kile Mungu alicho kitabili atakitimiza tu. Kutokana na unabii huu tunajifunza kwamba hivi karibuni Bwana yesu Kristo utarudi ili kuandaa mambo au mwenendo mwovu wa mwanadamu na kusimamisha njia za haki za duniani na hivyo kuleta furaha na amani kwa wanadamu

Ikiwa kama mada yoyote kati ya hizi tulizo zitoa hazijaingia ipasavyo akilini mwako; Unaweza ukalejea tena kwenye masomo na kujifunza tena kwenye Biblia; Muhtasari wa mafundisho makuu ya Biblia hupatikana mwishoni mwa kitabu hiki.

Lakini sasa swali limeimuka “Tufanye nini ?”

Hili sio swali jipya. Utakumbuka kwamba siku ya Pentekosti Petro alitoa hotuba yake kwa Wayahudi ambao walijihusisha kumsurubisha Yesu wa Nazareti akiwasibitishia kwamba Mungu alikuwa amefufuka kutoka wafu na kwamba kwasasa yuko mbinguni katika mkono wa kuume wa kuume wake akiwa mesia na Bwana. Katika hitimisho la hotuba yake wale walio kusanyika pale walimuuliza Petro “Tutendeje, ndugu zetu.” (Matendo 2:37 ). Jibu la petro likawa la moja kwa moja na lisilo la kosa : “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina Yesukristo mpate ondoleo la dhambi.” ( mstari wa 38 ). Hili ni jibu sahihi na la kueleweka kwa swali linalo mkabili mtakatifu mwaminifu wa kweli anaye panda kumtumikia Mungu kwa uaminifu kulikuwa takribani watu 3000 ambao kutokana na ujuzi wao wa injili na tamaa njema ya kutumikia Mungu viliwavuta kuitikia wito huu- na hivyo. “ Nao walilo lipokea neno lake wakabatizwa.”

Unaweza ukarejea tena kwenye masomo ba kujifunza tena kutoka kwenye Biblia, Muhsari wa mafudisho makuu ya Biblia huapatikana mwishoni mwa kitabu hiki.

Lakini sasa swali linainuka “ Tunafanyeje ?”

Hili siyo swali jipya utakumbuka kwamba siyo siku ya pentekosti Petro alitoa hotuba yake kwa wayahudi ambao walijihusisha katika kumsulubisha Yesu wa Nadhareth akuwa thitisha kwamba Mungu alikuwaamefufua kutoka katika wafu na kwamba kwa sasa yu Mbinguni katika mkono Kuume wake akiwa Mesiya na Bwana. Katika hitimisho la hotuba yake, wale waliokusainyika pale alimuuliza Petro” Tutendeje, ndugu zetu?”(Matendo 2:37) jibu la Petro lilikuwa la moja kwa moja na lisilo la kosa:”Tubuni mkabatizwe

Kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi " Mstari wa 38). Hili ni jibu sahihi na la kueleweka kwa swali linalo mkabili mtafutaji mwaminifu wa ukweli anaye panda kumtumikia Mungu kwa uaminifu. Kulikuwa takribani watu 3000 ambao kutokana na ujuzi wao wa Injili na tamaa njema ya kumtumikia Mungu viliwavuta kuitikia wito huu – na hivyo " Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa " (mstari wa 4) Paulo aliulizwa swali hilo hilo na mlinzi wa gereza kule Filipi baada ya tetemeko kulegeza minyororo ya wafungwa Paulo na Sila, Mlinzi aliuza; "Yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? " (Matendo 16:30) Swali hili muhimu humkabili kila mtu anayekuja kuelewa kuwa mwanadamu haishi milele na wote tuna dhambi mbele za Mungu. Pia jibu la Paulo ni la moja kwa moja kwenda kwenye lengo :"Mwamini Bwana yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako" (mstari wa 31)

Imani hiyo ilikuwa dhahili, kama inavyopaswa siku zote kuwa yaani kutaka kubatizwa katika Kristo. Hivyo tunasoma kwamba " kasha akabatizwa, yeye na watu wote wakati huo" (mstari wa 33). Yule mlinzi wa gereza, kama wale katika siku ya Pentekosti, kucheleweshа kuitikia wito wa neema ambayo Mungu alikuwa ameitoa kupitia Injili. Wakati huo huo" alitekeleza .

Yesu alitoa amri hii rahisi lakini ya muhimu kwa wafuasi wake.

Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Ingili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataoloka ; asiyeamini, atahukumiwa (Marko 16:15 – 16)

Masuala yaliyo mbele yako na kwa marafiki, kwa sababu ni masuala ya uzima wa milele au kifo. Unapoyaangalia mambo haya kwa undani tafadhali kumbuka kwamba tunapenda sana kukusaidia wewe zaidi kwa kadri tunavyoweza. Endapo kama una maswali yoyote au ungependa kujua zaidi kuhusu mada yoyote ya Biblia tafadhari tuandikie au tutumie barua pepe kwa kutumia anuani zilizo mbele ya kitabu hiki. Tamaa yetu ni kukusaidia wewe kuelewa ukweli wa neno la Mungu hivyo kuitikia wito na kujiandaa kumlaki Bwana Yesu Kristo katika ujio wake

**Marejeo kwa ufupi kuhusu ujumbe wa Biblia**

Sasa tumeshamaliza safari yetu ya kuipitia Biblia, ni vyema kuangalia tena mafundisho makuu ambayo Mungu ameyaweka katika neno lake. Ufuatao ni muhtasari wa mafundisho haya na kutokana na huu tunaweza kuona picha ya wokovu ambao Mungu ametoa – tumaini na furaha ya kushiriki hali ya kutokufa pamoja na Yesu Kristo katika ufalme ambao ataviimarisha mara atakaporudi.

Kwa kuorodhesha mafundisho haya tumetoa marejeo kutoa kwenye Biblia kuhusu mafundisho hili lililotolewa.

1.Biblia ni neno la Mungu lililopulizwa,ambalo Mungu aliwawezesha wanadamu kwa kupitia roho wake mtakatifu (2Petro 1:19 – 21; 2Timotheo 3:16; Warbrania 1:1 – 2)

1. Utimizo sahihi wa unabii wa Biblia ni wa uthibitisho wa uhakika kwamba Biblia ni neno la Mungu lililopulizwa (Isaya 46:9 – 10; Luka 24:25 – 27; Amosi 3:7; Daniel 2:28)
2. kuna Mungu mmoja tu wa kweli – ambaye ni Baba, na hakuna Mungu mwingine zaidi yake (Waefeso 4:6; 1 Wakorintho 8:4- 6; Isaya 45:5 – 6; Yohana 17:3,Kumbukumbu 6:4; Marko 12:29 – 32)
3. Mungu yupo milele na milele na ndiye chanzo cha uzima wa milele (Zaburi 90:2; 1Timotheo 6: 14 – 16; 1:17)

4. Mungu ni Mungu wa upendo, rehema, ukweli haki na utakatifu (Kutoka 34:6- 7, Zaburi 103; 1 Yohana 4:8 – 10; 1Petro 1:14 – 16)
5. Mungu aliumba mbingu na dunia na viumbe na mwanadamu juu yake (mwanzo 1:1 – 2, 2:7; Isaya 45:18; Matendo 17:24 Marko 10:6)
6. kusudi la Mungu la uumbaji ni kujaza dunia utukufu wake(Hesabu 14:21; Habakuki 2:14; Isaya 45;18; 1Wakorintho 15:28)
7. Nguvu ya Mungu ambayo hutumia kutimiza mapenzi yake huitwa Roho au Roho Mtakatifu (Zaburi 104:30; Mwanzo 1:2; Ayubu 26:13; 33:4; Zaburi 139:7 – 12)
8. ilikuwa kupitia hii takatifu ambayo Mungu aliwezesha Biblia kuandikwa na kuzaliwa kwa Yesu Kristo (2Petro 1:20 – 21; Luka 1:35)
9. Mwanadamu aliumbwa kutoka kwenye mavumbi ya aridhi kwa nguvu ya Mungu (Mwanzo 2:7; Ayubu 34:14 – 15 Zaburi 103:14)
10. Mwanamke wa kwanza, Eva, aliumbwa kutoka kwa mwanaume na Mungu kama mwenzi kwa mwanaume (Mwanzo 2:18 – 23; Mathayo 19:4 – 5
11. katika muungano huo wa Adamu na Eva Mungu aliweka kanuni ya msingi kwa ndoa (Mwanzo 2: 24 ;Mathayo 19: 3-9; Waefeso 5: 22-33 ).
12. Mungu alimueka Mwanadamu chini ya shelia kuto kuamini angeadhibiwa kwa kifo (Mwanzo 2: 16-17 ; Warumi 6:23 ).
13. Adamu alitenda dhambi kwakuto kumtii Mungu akamwadhibia kifo –yaani kurudi kwenye ardhi ambayo kwa iyo alipata kuumbwa. Hivyo mwanadamu akawa mtu wa kufa (Mwanzo 3:19; Warumi 5:12; 1Wakoritho 15:21 – 22)
14. kifo ni mwisho wa mambo yote – na hakuna ujuzi katika kifo. Wafu hawawezi kufikiri kumsifu Mungu au kuwa na kumbukumbu la Mungu (Zaburi 115 :17 ;6:5; 146:3 – 4 Mhubiri 9:5 – 6; Isaya 38:18 – 19)
15. Dhambi ni uasi wa sheria ya Mungu (1 Yohana 3:4; Zaburi 51:4)
16. Watu wote wametenda dhambi (Warumi 3:23; 1Yohana 1:9- 10)
17. Mwanadamu hujaribiwa kutenda dhambi na tamaa mbaya zitokazo (asili yake) moyoni mwake (Yakobo 1:14 – 15; 1yohana 2: 15; warumi 7;15 – 23; Waefeso 4:22; Warumi 7:15 – 20; Mwanzo 6:5; Yeremia 17:9 – 10)

**Mpango wa Mungu wa wokovu kwa mwanadamu mwenye mwili wa kufa.**

Mungu kwa hekima yake, aliusimamisha mpango ambao kwao dhambi ya mwanadamu ungesamehewa na angekuwa na tumaini la uzima wa milele.

Mpango huu ni pamoja na kumwinamia Yesu Kristo ambaye aliyekuwa “Mwana wa Mungu na Mwana wa Adamu”

18. Adamu na Eva walipotenda dhambi, Mungu aliahidi kumtoa “Uzao” wa mwanamke ambaye angeshinda dhambi na kutoa njia ya wokovu. Uzao huo ulioahidiwa ni Yesu Kristo (Mwanzo 3:15; Luka 1:35; Wagalatia 4:4; Mathayo 1:21)
19. Mungu alimuahidi Abrahamu kwamba uzao wake ungerithi nchi milele na kupitia yeye mataifa yote yangebarikiwa. Uzao huo ni Yesu Kristo (Mwanzo 12: 1- 3; 14 – 17 22:18; Wagakatia 3:7 – 8, 16,26 – 29; Luka 13:28)
20. Mungu alimwahidi Daudi kwamba angekuwa na mzao au mwana ambaye angekuwa pia mwana wa Mungu .Huyu mwana aliyeahidiwa ni yesu kristo ambaye atarudi duniani na kutawala juu ya ufalme wa Mungu milele (2Samweli 7:12-16:Luka 1:3-33:matendo 13:22-23 ufunuo 5:5:22:16 Yeremia 23:5-6)

21. Ahadi ya kuzaliwa na kazi ya yesu krsto ilitabiriwa katika sehemu zingine katika Biblia –mfano kwa Musa (kumbukumbu 18:18-19 angalia matendo 3:22-26 ) na kwa Isaya (Isaya 7:14:angalia Mathayo 1:21_23)
22. Kutokana na ahadi hizi muda uliopowadia Mungu alimtuma malaika wake Galbneli kuja kumpasha maria kwamba angechukua miamba ya mwana kwa uweza wa Roho Mtakatifu wa mungu ambaye angeitwa yesu.Ambaye pia angekuwa Mwana wa Mungu (Luka 1:30-350.
23. Ingawa Yesu kristo alizaliwa kwa uweza wa Roho mtakatifu wa mungu alikuwa mwanadamu wa mwili wa kufa akiwa na maumbili ya mwili na damu kama ya maana yake maria (1Timotheo 2:5 Matendo 2:22 Waebrania 2:14: ! wakorintho 15:21)
24. akiwa mwana wa Mungu alipewa nguvu katika kuelewa njia za Mungu na katika maisha yake ya utiifu mkamilifu aliifuma tabia ya Baba yake kwa watu wote ilikuifuata (isaya 11:1-4:50:4 Yohana 12:49 -50 17 :6:14:9)
25. Kwa sababu alikuwa na maumbile kama yetu alijaribiwa kwa namna yeyote ile kama watu wengine-ila tu hakuwahi kutenda dhambi bali siku zote alikuwa akifanya mapenzi ya Mungu (Waebrania 4:15:2:18; yakobo 1:14!petro 2:22-23; Mathayo 26:39; Mathayo 16:22-23).
26. katika kusubuliwa kwake yale maumbile ambayo alikuwa nayo yaliyo katika watu wote yaliharibika (waebrania 2:14:wafilipi 2:8-9warumi 8;3)
27. Kwa sababu ya maisha utiifu mkamilifu haikuwa haki kubaki katika wafu na kumpa maubile ya kutokufa (Matendo 2:24; warumi 5:15,19; warumi 6:9)
28. Kupitia adamu dhambi na matokeo yake vilikuja –kifo .kupitia utiifu mkamilifu wa yesu kristo mpaka kifo matokeo yake ikawa ufufuo kutoka katika wafu (1Wakorintho 15:21-22
29. Baada ya ufufuo wake yesu alipaa mbinguni na kwa sasa yuko katika mkono wa kuume wa Mungu (Matendo 1:10-11;zaburi 110:1,Matendo 2:32-35).
30. Yesu kristo ataridi hapa duniani kuja kuimarisha ufalme wa mungu (matendo 1:10-11:Ufunuo 11;150
31. Mwanadamu ana mwili wa kufa –hana nafsi isiyokufa kwa asili. Tumaini pekee kwa mwanadamu ni ufufuo kutoka katika wafu yesu kristo akirudi (1 wakorintho 15:21-23: Yohana 5:28-29:Yohana 11:24:2Timotheo 4:1:1Wathesalonike 4:14-18)
32. Wokovu kutoka katika dhambi na kifo hutolewa kwa wale tu ambao wameelewa Injili, kuiamini kutubu na kubatizwa katika Yesu kristo (Marko 16:15-16)
33. Ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu (matendo 2:38:22:16)
34. Ubatizo hufanyika kwa kuzamishwa katika maji (matendo 8:38-39;10:47;Yohana 3:23)
35. Ubatizo ni alama ambapo tunahusianisha kifo na ufufuo wa Yesu kristo (warumi 6:3-6)
36. Baada ya ubatizo mwanafunzi hutembea katika njia ya maisha akifuata kielelezo cha kristo (warumi 6:4-6;waefeso 4:22-24)
37. Baada ya ubatizo mwanafunzi ana uhuru wa kumkaribia Mungu kwa maombi kupitia Yesu kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi anazoweza kutenda (1Yohana 2:1;warumi 8:34;Waebrania 4;14-16)

INJILI- HABARI NJEMA ZA UFALME WA MUNGU NA WOKOVU KUPITIA YESU KRISTO.

Neno Injili maana yake “Habari njema “na inahusu tumaini la wokovu kutoka katika dhambi na kifo kupitia yesu kristo na kuja kwa ufalme wa Mungu ambao atausimamisha hapa duniani (matendo 8:12;Marko 16:15-16)

38. Ufalme wa Mungu ulioudolewa kutoka kwa waisrael kwa sababu ya upungufu wa imani yao hata hivyo bado ni mashahidi wa Mungu na watakuwa na sehemu katika ufalme wa Mungu ujao (Ezekieli 21:27;Mathayo 21;43;Isaya 43:12;yeremia 33”:25-26;matendo 1:6-7;matendo 3;21;Ezekieli 36:22-29;mathayo 19;28)
39. Yesu kristo atarudi hapa duniani akiwa mwenye mwili na kuonekana.Atakuja kuimarisha ufalme huu (matendo 1;10-11;!wathesalonike 1:10;1wathesalonike 2:19:ufunuo 22:12)
40. Yesu kristo atakaporudi kwanza atawafufua wale ambao wamezijua njia za mungu .watakusanya pamoja kwa ajili ya hukumu kutia ndani waliohai na kujua injili (1wakorintho 15:21-23;Danieli 12:1-3;Yohana 5:28-29 ;Yohana 11:24;2timotheo 4:1;warumi 14:10-12;2wakorontho 5;100
41. waaminifu watapata nafasi katika ufalme wa Mungu na kusaidia kutawala wakiwa chinmi yesu kristo akiwa mfalme (Mathayo 25:34;Luka 19:17 Ufunuo 5:10)
42. Waaminifu watapewa mwili wa kutoka na wasiotii watakataliwa (1 wakorintho 15:52-54;Danieli 12:2-3 luka 20:35-36;Mathoyo 25:21,30)
43. Ufalme huu utaimarishwa hapa hapa duniani utazibadili falme zote za sasa na mifumo ya utawala (danieli 2:44;Mathayo 6:10;ufunuo 11:15)
44. Makao makuu ya ufalme huu yatakuwa yerusalemu ambako yesu kristo atatawala kama mfalme (Yeremia 3:17;isaya 2:2-4Zekaria 14:16-17;Mathayo 5:35;Zekaria 14:9)
45. Yesu kristo atakaporudi Yerusalemu wayahudi waishio nchini humo ndipo watakapomkiri kuwa mesiya 9masihi )na mfalme wao (zekaria 12:10;13:6;Mathayo 23:39)
46. Wayahudi wengine walitawanyika watarudishwa katika nchi ambayo mungu alimwahidi abrahamu nao pia watamkiri Yesu kuwa masihi wao (Yeremia 30:10-11;31:31-34;Zekaria 8:7-8warumi 11:25-27)
47. Ufalme wa Mungu utadumu kwa kipindi cha ukileta amani usalama na furaha kwa watu wote kupitia utawala wa haki wa yesu kristo na wafuasi wake waaminifu (Isaya 32:1-17;35:10;zaburi 12:ufunuo 20:4-6)
48. Mwisho baada ya miaka 1000 kuisha dhambi na kifo vitakuwa vimeondolewa kabisa na dunia atajwa na utukufu wa mungu (Habakuki 2:14;Ufunuo 21:1-5)

**AMRI ZA KRISTO**

1. Wapendeni adui zenu fanya mema kwa wakuchukiao (Mathoyo 5:44)
2. Usiziwe uoni mtu akikupiga shamu moja mgeuzie na lingine (mathayo 5:39,40)
3. Msijilipize kisasi bali iacheni ghadhabu upite niafadhali kudhurumiwa (warumi 12:18-19;1wakorintho 6;70
4. Mtia akikunyanganya vitu vyako usiombe akurudishe (luka 6:29-30)
5. patina na mshitaki wako upesi ukinyenyekea hata kama si kosa lako kwa ajili ya amani (mathayo 5:25;1wakorintho6;70

6. Usifanye kazi ili kuwa tajiri kuwa tayari kwa kila kazi njema wape wakuombao wasaicheni wanaonewa (1Timotheo 6:8;warumi 12;13;waebrania 13:16;yakobo 1:27)
7. msifanye wema wenu machani pa watu Basi wewe utaona sadaka usiopige pande mbele yako mkono wako wa kushoto usijue mkono wako wa kuume unachokifanya (mathay 6:1-4)
8. usimlipize mtu ovu kwa ovu ushinde uovu kwa jema (warumi 12:17)
9. wabarikini wanaowalaam laana isitoke kabisa vinywani mwenu (mathayo 5:44;warumi 12:14)
10. Usimrudishe mtu ovu kwa ovu au laumu kwa laumu bali wenye kubariki (1 petro 3:90
11. waebrania wanaowaudhi (mathayo 5:44)
12. msimugunukiane :msihukumu;msilaum;(yakobo5:9;mathayo 7:1)
13. wekeni mbali hasira uchungu na lugha yote chafu (waefeso 4;31;1petro 2:1)
14. Ungani dhambi namna ya dunia hii;msiipende dunia (warumi 12:2;1yohana 2:15)
15. kataa ubaya na tamaa za kidunia (Tito 2:12;mathayo 5:30)
16. watumwa watuni wale walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili hata kwa mabwana wabaya (waefeso 6:5-80)
17. Msinie makuu bali jishughulishe na mambo yaliyo manyonge (warumi 12;16)
18. Msiwiwe na mtu chochote (warumi 13:7-8)
19. Kama ni dhambi (kama unafahamu au kusikia 0usione kwa wengine bali mwambie ndugu aliyekosa kuhusu jambo hilo kati yako nay eye tu kwa lengo la kupatanisha (mathayo 18:15;wagalatia6:1)
20. Mpende bwana mungu wako kwa moyo wako wote (mathayo 22:37)
21. Ombeni kila siku bila kukata tamaa ombeni kwa siri (luka 18:1 mathayo 6:7)
22. Mshukuruni mungu kwa kila jambo na mjua Mungu katika njia zako zote (waefeso 5:20;mithali 3:6)
23. Yoyote myatakayo mtendewe na watu nanyi watuendeni vivyo hivyo (mathyo 7:12)
24. Fuateni kielezo cha kristo na mfuate nyayo zake (1petro 2:21)
25. kristo akae kwa mingi ndani ya miyo yenu kwa maini (waefeso 3:170
26. Mpende kristo zaidi ya mambo yote ya dunia naam hata nafsi yako mwenyewe (luka 14:260
27. Mkiri kristo mbele za watu (luka 12 :8)
28. Jihadharini mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi na ulevi na masumbufu ya maisha haya yasije yakadhaoofisha maoni yenu (luka 21:34-36;mathayo 24;44)
29. Mpende jirani yako kama unayojipenda (mathayo 22:390
30. Usijiweke ukuu kwa kila mmoja (mathayo 23;10-12)
31. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe bali kila mtu aangalie mambo ya wengine (wafilipi 2:4;wagalatia6:20
32. Nuru yenu na iangaze mbele za watu lishikeni neno la uzima Fanyeni mema mbele ya watu wote kila mpatapo nafasi (mathayo 5:16; Wafilipi2:16; wagaratia 6:10 ).

33. Kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, udanganyifu usio na kati ya kizazi chenye ukaidi (wafilipi 2:15 ).
34. Kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu awezaye kuwaonya watu kwa upole mwenye huruma na mwenye kusamehe (2Timotheo 2: 24; Tito 2:2; Waefeso 4: 32).
35. Muwe na kiasi na kukesha waamiifu na wapole (Wafilipi 4:5; 1petro 1:13; 5:8).
36. Uvueni uongo na mkaseme kweli kila mtu na jilani yake . wekeni mbali uongo wote (Waefeso 4: 25 ).
37. Lolote mfanyalo lifanyeni kwa moyo kama kwa bwana wala si kwawanadamu (Wakorosai 4:23 )
38. Kesheni simama imara katika imani yanyeni kiume mkawe hodari furahini katika bwana siku zote ( 1wakolitho 16:13; wafilipi 4:4; wathesolanike 5: 6-10).
39. Jivikeni moyo wa rehema, unyenyekevu, upole , uvumilivumkichukiana na kusameheana (Wakolosai 3: 12 ; Warumi 12:12)
40. Fuateni amani na watu wote (waebrania 12: 15 )
41. Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao (Warumi 12:15 ).
42. Fuateni mambo yote yaliyo ya kweli, yoyoteyaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki yoyote yaliyo safi, Yoyote yenye kumpendeza, yoyote yenye sifa njema ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote (wafilipi 4:8).
43. Ukimbieni uwasherati uchafu wowote wa kutamani, ulevi, aibu, maneno ya upuuzi na ubishi (Waefeso 5:3-4)
44. Lolote ulifanyalo fikilia matokeo yake kwa kuliheshimu jina la Mungu kwa watu , Fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu (1wakoritho 10:31, 3:17)
45. Jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi. Hivyo muwe hai kwa ajili ya nafsi zenu wenyewe bali kwaajili yake yeye aliye kufa akafufuka kwa ajili yao (Warumi 6: 11; Wakoritho 5:15 )
46. Muwe na juhudi katika matendo mema, bila kuchoka siku zote mkidumu katika kazi ya Bwana. (Tito 2:14; Wagaratia 6:9 )
47. Usimtukane mtu yeyote (Tito 3:2 )
48. Neno la kristo likae kwa wingi mioyo yenu (Wakorosai 3: 16 )
49. Maneno yenu yawe na neema siku zote (Wakolosai 3: 8; 4:6 )
50. Nyenyekeeni kwa wenye uwezo na mamlaka na kutii na kuwa tayari kwa kila kazi njema watiini watu wenye mamlaka kwaajili ya bwana (Tito 3: I )
51. Iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote (1petro 1:15-16)
52. Usimpe adui nafasi ya kulaaumu (1 Timotheo 5:14 )ili kusaidia zaidi katika kuelewa kwako misingi rahisi ya mafundisho ya Biblia
    Tunatoa kitabu cha ( kiingeleza )

(BIBLILIA INACHOFUNDISHA.” Imani ya wa christadelphian)

Kitabu hiki hushughurikia mafundisho ya msingi ya Biblia ya somo kwa somo mpangilio mzuri na wakueleweka. Maneno ya Biblia ya mekusanywa kwa kila somo na kuchapwa kwa ujumla wake na hivyo unaweza kuona nguvu ujumla wa Biblia wewe mwenyewe. Mwishoni mwa kitabu kuna orodha ya maneno yaliyo pangwa kwa mjibu wa alfabeti ya maada zilizomo na orodha ya manukuu yote kutoka kwenye Biblia kwaajili ya urahisi katika kufanya marejeo.

Kitabu hiki ni zana nzuri ya kukusaidia kupata wazo kuu halisi la Biblia inacho fundisha.

Baadhi ya maada 27 zilzomo katika kitabu hicho ni

.KRISTO- Mwana wa nani Yesu mtakatifu Yesu na Ibil Ufufuo na hukumu Hili ni fumbo la Israeli Ishara za kurudi upesi kwa kristoUfalme wa Mungu utafanana na nini?kwanini ningebatizwa ? Mfuasi wa Yesu na ulimwengu. Baada ya kupitia kozi ya kuichambua Biblia mwalimu wako atapenda takusaidia kwa kutumia kitabu hiki kingine Sura baada ya Sura na kujibu maswali yote ambayo waweza kuwa nayo. Kama unataka nakara moja itumwe kwako wasiliana na mwalimu wako wa kozi ya kuichambua biblia ("UVUMBUZI WA BIBLIA ) au kwa : EXPLORING THE BIBLE . P.O BOX 20, MODBURY NORTH 50092 SOUTH AUTRALIA, AUSTRALIA

Email: Bible @exploingtheBible. Net

Biblia pia inacho fundisha na pia hupatikana kwa kupitia maktaba za christadelphians ulimwenguni pote. Kitabu kimetafasiriwa na kaka Rphael Mkeya wa ekelesia ya Mlowo- Mbozi ; Mbeya; Tanzania .

Email Simumkeya@yahoo.com.